**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0620273708/0783258400**

**Makamu Mkuu wa Shule:0719301139/0683163790**

**Mwl wa bweni: 0686028722**

**Shule ya Sekondari KANADI**

**S.L.P: 473 - BARIADI**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA……… KATIKA SHULE YA SEKONDARI KANADI HALMASHAURI YA ITILIMA MKOA SIMIYU MWAKA…………………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika. Shule hii mwaka……………… na atasoma tahasusi ya …………………. Shule ya Sekondari **Kanadi** ipo umbali wa Kilometa 37 Mashariki mwa Mji wa Bariadi. Usafiri wa basi kutoka mjini Bariadi unapatikana katika kituo cha mabasi <u>Bariadi -</u> <u>Somanda</u> Nauli ni Shilingi 6,000/= kwa basi na Shilingi 12,000/= kwa pikipiki.
Muhula wa Masomo unaanza baada ya Waziri wa Ofisi ta Waziri Mkuu -TAMISEMI kutangaza tarehe ya kuanza kwa muhula wa masomo.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali dark bluu mbili (2) zenye marinda mawili kila upande **isiwe model** kwa ajili ya darasani*;*
ii. Mashati mikono mirefu mawili (2) kwa ajili ya darasani.
iii. Sare ya Michezo ni bukta ya bluu mbili (2) na raba rangi yoyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta ya bluu moja;
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali ya kijivu moja au zaidi, track suti bluu moja au zaidi **isiwe model.**
ix. Tai dark bluu ndefu mbili (2).
x. Tisheti (T-shirt) kijivu na nyekundu kwa ajili ya kushindia zisizo na maandishi yoyote.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

i. Madaftari ya kutosha (counter book quire 3) kulingana na idadi ya masomo katika mchepuo aliopangwa;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Aje na godoro futi 2 ½ kwa 6;
vii. Mashuka Jozi 2rangi ya pink,foronya ya godoro 1 ya pink,na chandarua 1*;*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 1 ndogo na moja kubwa (lita 20) zenye mifuniko(HGLi, HKL, HGL, PCB na PCM);
xi. Kwanja 1(HGLi, HKL, HGL), jembe 1 lenye mpini (HGLi, HKL, HGL, PCB na PCM), reki 1(PCB na PCM), mifagio 2 (soft bloom na moper) wa ndani (PCB na PCM) na nje (HGLi, HKL, HGL).

### 2.3 Michango mbalimbali Shule ya Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Michango yote iwekwe kwenye akaunti ya shule kwa jina la **KANADI SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION ACCONT – 30501100019** benki NMB **mwanafunzi asije na pesa shuleni haitapokelewa.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi**
- **kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………Kidato cha ……..… Baada ya kusoma kwa makini na kuelewa sheria za shule na ahadi za mwanafunzi zilizowekwa Na Uongozi wa shule. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu pamoja na Mkuu wa Shule kuwa nitazitii; kuzingatia; kutekeleza na kufuata sheria zote za shule na kwamba nikizivunja sheria za shule nijihesabu nimejifuta shule mwenyewe.

Jina kamili na sahihi ya mwanafunzi………………………………..……Tarehe…………………………………….
Jina kamili na sahihi yaMzazi/mlezi wangu……………………..…………………. Tarehe………
Namba ya simu ya mzazi/mlezi …………………………

Taja jina la mtu wa karibu ambaye shule inaweza kuwasiliana nae kwa jambo lolote iwapo mzazi/mlezi akikosekana.………………………………. Anwani…………………………………………………. namba yake ya simu……………………….

Jina na sahihi ya Mkuu wa Shule ……………………………. Tarehe ……………………

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART‘A’

FROM the Headmatser

TO THE MEDICAL OFFICER

…………………………… ………………………

……………………………………………………..

Mr.……………………………………………………(Name in full)

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect

I (a) Eyesight
(b) Venereal Diseases

(c) Hearing
(d) Leprosy (c) Speech
(e) Epilepsy (d) Limbs
(f) TB
II Neuroses

III Other serious diseases

Date…………………………………Signature………………………………

PART B: MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by a

Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight…………………… (e) Venereal Diseases…………………

(b) Hearing……………………. (f) Leprosy……………………………...

(c) Speech……………………. (g) TB …………………………………..

(d) Limbs……………………

II Neuroses…………………………………………………………………….................

III Other serious diseases ……………………………………………………………………..

Date…………………………………………Signature…………………………….......
Station……………………………………... Designation………………………………

VITABU ANAVYOPASWA KUWA NAVYO MWANAFUNZI

| MATHEMATICS | ENGLISH | GEOGRAPHY | BIOLOGY | CHEMISTRY | PHYSICS |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Advanced maths by L.K.Turner I & II, 2. Advanced maths by C.J.Tranter, 3.Advanced maths by L.K.Shayo, 4. Advanced maths by Backhouse Vol.I & II. 5.Advanced maths Vol.I & II 6.Understanding Mathematics 7.Electronic Calculator (Scientific Function 1991) | 1. Advanced literature by Nyambari Nyangwine 2. The real English Advanced Level by Dr.Michael Kadeghe 3. New Advanced Level English by Charles .E. Shalua 4. Introduction of Phonology by Gimson 5. A University Grammar of English 6. A complete English course for Form V & VI by Dr.Michael Kadeghe 7. Oxford Advanced learners Dictionary | 1. A practical Guide to Statistical Maps and Diagrams by H.C.Truran 2. Practical Geography for Africa by J.M.Pritchard 3. Principles of Physical Geography by F.J.Monkhouse 4. Human and Economic Geography by G.C.Leong and G.C. Morgan 5. Map Reading by Zisti Kamili 6. Photo Interpretation by kura 7. Physical Geography ALevel by D.T .Msabila 8. Physical Geography by R. Bunnet | 1. Biological Science by Taylor et al (Cambridge) 2. Advanced Biology by Sinpkins (ELBS) 3. Understanding Biology by Co Susan Trole 4. Understanding Biology by Nelson Thornes | 1. A level chemistry by (E.N.Ramsden) 2. Advanced level Inorganic Chemistry Part I & II 3. Organic Chemistry Part A & B by Tanzania Publishing House 4. Physical Chemistry by Mzumbe 5. Advanced Level Chemistry by Ramsden | 1. Advanced Level Physics by (M.Nelkon & P.Parker), 2.Concise "A"Level Physics By (Arwahyses), 3.Physics by (Tom Duncan), 4.New Intermediate Physics, 5.Rodger Muncuster by (Rodger Muncuster), 6.Calculation of Advanced Level Physics by (Tllower and J.F.Rounce). |
| **HISTORY** | **KISWAHILI** | | | | |
| 1.Advanced level History for form Five and SIX by Oxford 2.Advanced level History paper 1&2 by Z.Kamili 3.The Evolving world by Denis Ngalula | 1.SAMAKIS A na SAMAKISA vya Masmaba na Wenzake 2.Kiswahili Kidato cha Tano na Sita by Oxford 3.Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 | | | | |

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KANADI

ZACHARIA ANGELO NOGU

MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
KANADI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 473- BARIADI

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0783258400 au 0620273708**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0717301139 au 0683163790**
- **Mwandamizi Taaluma : 0657646267**
- **Mwandamizi Malezi : 0688324210**